
NOVEMBA 2019
MAKALA MAALUM

LINDA ARDHI YA MWANAMKE



# KAMPENI YA MWANAMKE KUPATA HAKI YA KUMILIKI ARDHI

## *Mwanamke atakavyopata haki ya kumiliki ardhi*




TANZANIA imechaguliwa na Umoja wa Mataifa kuwa nchi ya kwanza kufanya kampeni ya kuhakikisha mwanamke anapata haki ya kumiliki ardhi kama ilivyo kwa wanaume.

Kampeni hii ni endelevu inafanyika kwa miaka 12 kuanzia mwaka 2019 hadi 2030 na inatarajiwa kuzinduliwa Novemba 21,2019 jijini Dar es salaam na Waziri wa Afya,Jinsia,Maendeleo ya Jamii,wazee na watoto Ummy Mwalimu.

Wadau 25 kutoka Taasisi mbalimbali wanashiriki katika kampeni hii likiwemo Shirika la kimataifa la Landesa ambalo ni Taasisi inayoshughulikia maendeleo vijijini na wanahabari ambao watasaidia kufanikisha kampeni hii kuwafikia watu wengi .

Godfrey Massay ni Mwanasheria na Mtaalam wa masuala ya ardhi kutoka Taasisi ya Landesi ardhi ambazo zinakabiliwa na changamoto katika utekelezaji wake hivyo kusababisha baadhi ya watu kama wanawake kukosa haki za kumiliki ardhi .

“Tanzania imechaguliwa kuwa ya kwanza na Umoja wa mataifa kuona namna ya kuwasaidia wanawake kumiliki ardhi kwa sababu,ardhi ni maisha na kila kitu,sera na sheria nzuri zilizopo zinatakiwa zitekelezeke’’,anasisitiza Massay.

Hata hivyo anaitaja sababu ya Tanzania kuchaguliwa kuwa nchi ya kwanza kutekeleza kampeni hii kuwa ni kutokana na utashi wa serikali uliopo na kampeni zilizofanyika siku za nyuma kama Mama Ardhi kupata mafanikio makubwa.

Akizungumza wakati anatoa mafunzo maalum kwa wanahabari takribani 20 waliochaguliwa katika nchi nzima kujifunza habari zinazohusiana na haki ya mwanamke katika ardhi na uwekezaji wajibifu,Massay anasema mafunzo hayo yanatolewa kwa wanahabari kwa sababu wana namna nyingi za kufikisha ujumbe katika jamii.

Anasisitiza kuwa wakati sasa umefika duniani kote kuhakikisha mwanamke anapata haki ya kumiliki ardhi na kwamba hapa Tanzania kuanzia Katiba ya nchi ya mwaka 1977 hadi sheria ya ardhi ya mwaka 1999 kifungu cha nne na tano vinampa nafasi mwanamke kumiliki ardhi. ***Inaendelea uk 2***

# Mwanamke atakavyopata haki ya kumilki ardhi



Hata hivyo Mtaalam huyo wa anaitaja changamoto kubwa ambayo inasababisha sheria za ardhi kushindwa kutekelezeka ni baadhi ya mila na desturi zilizopo hapa nchini zinamkandamiza mwanamke.

Anasisitiza kuwa sheria ya Tanzania inamruhusu mume na mke kumiliki ardhi ili mradi tu wawe wamefunga ndoa zinazofahamika ikiwemo ya kidini,serikali,kimila au asili na kwamba ni vema wanandoa kuwa na tabia ya kuandika wosia kabla ya kifo ili haki iweze kupatikana kwa mjane.

Khadija Mrisho ni Mwanasheria na Mtaalam wa ardhi kutoka Taasisi ya Landesa anasema kutokana na changamoto zilizojitokeza kwa mwanamke kumilikishwa ardhi duniani kote,wadau mbalimbali wa kimataifa waliamua kufanya kampeni ambayo ilitajwa kwa mara ya kwanza jijini London nchini Uingereza mwaka 2018.

Anasema kampeni hii inatarajia kuzinduliwa nchini Tanzania Novemba 21,2019 na Waziri Ummy Mwalimu lengo likiwa ni kuvutia wadau mbalimbali wa maendeleo, wataalam wa teknolojia na Taasisi za utafiti wa haki ardhi za wanawake.

“Kampeni hii ni ya miaka 12 inaanza 2019 hadi 2030 inakwenda sanjari na malengo ya maendeleo endelevu,tathmini itafanyika baada ya miaka mitatu’’,anasema Mrisho.

Anataja sababu iliyosababisha kufanyika kwa kampeni hiyo kuwa ni kutokana na umuhimu wa mwakamke katika jamii ambapo katika baadhi ya watu wanamuona mwanamke ni kama Waziri wa Mambo ya Ndani,pia ni nguzo ya familia hivyo anastahili kupata haki ya kumilikishwa ardhi ili kuounguza umaskini katika jamii.

Hata hivyo anasema kampeni hiyo ni ya kimataifa inajumuisha Taasisi na mashirika 25 ya kimataifa na kwamba ili kuhakikisha kuwa utekelezaji unafanikiwa wameshirikishwa wadau wa maendeleo na kwamba kauli mbiu yake inasema *Linda ardhi ya mwanamke wa Tanzania.*

Kulingana na Mrisho maono baada ya kampeni,ni kuona jamii ya Tanzania inapata jamii ya wanawake na wanaume wenye haki ya kumiliki na kutumia ardhi kwa usawa bila



# Kampeni ya  kumwezesha ,mwanamke wa Tanzania kupata haki ya kumilikishwa ardhi

**KAMPENI YA MWANAMKE KUPATA HAKI YA KUMILIKI ARDHI NCHINI TANZANIA INAFANYIKA KWA MIAKA 12 KUANZIA 2019-2030**




Anasema katika kipindi cha kampeni lengo ni kuhakikisha kuwa changamoto zilizopo katika sera na sheria  za ardhi zinajengewa uelewa katika umiliki wa ardhi sawa kwa wote,kuchochea na kulinda haki za ardhi kwa mwanamke na watanzania kwa ujumla wake.

Kwa mujibu wa Mrisho mkakati wa kampeni hiyo una malengo manne ambayo ni kuondoa mila na desturi zinazomzuia mwanamke kudai haki ya ardhi na kuchochea matumizi ya ardhi kwa ajili ya kumuinua mwamke kiuchumi.

Anaitaja mikakati mingine kuwa ni kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye vyombo vya maamuzi na kuangalia haki za ardhi za mwanamke kwenye uwekezaji mkubwa katika ardhi.

“Tunatarajia kupata matokeo makubwa baada ya kampeni hii ikiwemo kuwa na ongezeko na wanawake wanaodai haki ya kumiliki ardhi,kuboresha uchumi wa mwanamke na kupungua idadi ya wajane ambao hawamiliki ardhi’’,anasisitiza.

Anawaja walengwa katika kampeni hiyo kuwa ni machifu,viongozi wa jadi,viongozi wa dini,vyombo vya habari,Taasisi za utafiti na wanataaluma na kwamba kazi zitakazofanyika kwenye kampeni ni kujenga majukwaa,kutumia vyombo vyote vya habari,na mitandao,kuandaa vijarida na vipeperushi vya haki ardhi na kutumia wadau mchanganyiko.

Eda Sanga ni mwanahabari mkongwe na mmoja wa watoa mada katika mafunzo anatoa rai ili kufanikisha kampeni hiyo wanahabari wazingatie uongozi na ubunifu unaoendana na vionjo vilivyopo sasa katika utoaji habari.

Kampeni imekuja wakati  wa agenda ya maendeleo endelevu ya 2030 ambayo utekelezaji wake unashirikisha nchi zote na wadau wote ambao

IMEANDALIWA NA
ALBANO MIDELO

**MWANDISHI WA HABARI KUTOKA SONGEA MKOANI RUVUMA**

**S.L.P 600 SONGEA**

**SIMU 0784765918**

**NAFANYAKAZI KATIKA VYOMBO VYA HABARI VIFUATAVYO**

**1.TANZANIA STANDARD NEWSPAPER**

**2.SONGEA TV ON LINE**

**3.PERAMIHO PUBLICATIONS**

**4..MITANDAO YA KIHABARI**

***Naitwa Albano Midelo ni Mwandishi wa habari Mwandamizi ambaye nafanyakazi katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.***

***Huduma za kihabari ambazo tunaweza kukuhudumia ni***

***1.kuandika makala mbalimbali***

***2.kuandika habari za matukio mbalimbali***

***3.kutengeneza matangazo na kuyatangaza***

***4.kuandaa vipeperushi,newsletter,documentary na info graphics***

# *Kampeni ya mwanamke kupata haki ya kumiliki ardhi*



wanatakiwa kutekeleza malengo endelevu 17,shabaha (target) 169 na viashiria(indicators) zaidi ya 238.

Jambo la kufurahisha ni kwamba miongoni mwa agenda za maendeleo endelevu,kuna malengo yanayozungumzia haki ya kumiliki ardhi kwa mwanamke hivyo kuleta mapinduzi makubwa katika kuelezea haki ya mwanamke kumiliki ardhi.

“Kati ya indicators 238 saba zinazungumzia ardhi,tatu kati ya saba zinazungumzia haki ya kumiliki ardhi kwa mwanamke, kiashiria cha kwanza ni 1.4.2 kinazungumzia umiliki wa ardhi kati ya mwanamke na mwanaume na kuwepo kwa taarifa za watu wote wazima wenye uhakika wa umiliki wa ardhi'',anasisitiza Godfrey Massay Mtaalam wa Landesa.

Anabainisha zaidi kuwa kifungu hicho kinataka haki ya kumiliki ardhi itambuliwe na makundi yote na mahakama itoe haki ya muda mrefu.

Kiashiri cha pili kilichopo katika maendeleo endelevu anakitaja kuwa ni 5.a.1 ambacho anasema kinataka taarifa za umiliki wa ardhi za kilimo na kwamba kiashiri cha tatu anakitaja kuwa ni 5.a.2 ambacho anasema kinaangalia idadi ya nchi zinazotoa haki sawa wa umiliki wa ardhi kwa wanawake.

Mtaalam huyo kutoka Taasisi ya Landesi anasema taarifa za watanzania wanaoruhusiwa kumiliki ardhi zipo katika tovuti ya Idara ya Takwimu TBS na kwamba Tanzania imekuwa nchi pekee duniani hadi kufikia Mei 2019 kuwa na watu wanaoruhusiwa kumiliki ardhi.

Haki ya mwanamke kumiliki ardhi nchini Tanzania inawezekana tuhakikishe sera na sheria nzuri zilizopo zinatekelezwa.